# Tutakuwa na furaha kama... tutakuwa na ujasiri wa kugawanya!

"Heri masikini wa roho maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Mt. 5,3)

## Lengo

Kufufua ushirika wa vitu, wa kiroho na wa vipaji, katika ngazi ya mahali na ngazi ya dunia

## Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mang'amuzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"



## Shughuli ya utambulisho

**Mchezo wa ushirika wa problem solving "ARRAFFA"**

**MUDA:** dakika 30/saa 1

**VIFAA:** chumba kimoja na meza kubwa, vigingi vingi vya kutosha vya vifungo au maharage, karatasi kubwa yenye sheria za mchezo.

**UENDESHAJI:** wachezaji 10 wanaizunguka meza na wanaobaki wanasimama nyuma yao kama watazamaji. Wachezaji wanawekewa mezani vigingi 22 kwa ajili ya mchezo. Sheria za mchezo zinasomwa na kueleza kuwa mchezo unapoanza vijana wanaweza kuchukua vigingi, lakini vile vitakavyobaki mezani vitaongezwa mara mbili. Atashinda atakayepata vigingi 24. Mizunguko kadhaa itarudiwa mpaka vijana watakapoelewa kuwa wote wanaweza kutajirishana lakini kidogo kidogo.

**PENDEKEZO:** lazima kurudia mchezo mara kadhaa ili kufikia hitimisho kwamba inatosha kutuliza kiu ya kunyakua ili kumpa kila mtu nafasi ya "kushinda." Sindikizeni mchezo huo kwa tafakari na kutiana moyo kiasi kwamba utatuzi utatoka kwa vijana wenyewe.

**RIPOTI FUPI:** mwishoni mwa mchezo yataendeshwa majadiliano ya uchunguzi juu ya masuala ya tofauti ya rasilimali duniani, kutegemeana na utamaduni. Ni lazima kufaulu kulifikia wazo la kuushinda ubinafsi/ mkusanyiko wa kikabila ili kuwa na uwazi wa kugawana.

*Kutoka kwenye "Mchezo wa uchumi", M. Morozzi, A. Valer, ed EMI 2001*

## Tuishi hivi

Utamaduni wa kutoa unaweza kugeuza vijiji vizima. Kama ilivyotokea Esmeraldas, eneo la Equador ambako masiki wapo karibu asilimia l'8 ya idadi ya watu wote. Nyumba ni za miti, hakuna maji safi ya kunywa wala shule. Ukosefu wa kazi unaongezeka na kusababisha ulevi. Vijana wengi wa umri wetu kwa kutokuwa na mwelekeo wanajiingiza kwenye uhalifu.




Tulipowafahamu vijana wa eneo lile tulienda kuwatembelea. Tulianza nao urafiki ambao unaendelea hata kama kuona hali yao ya maisha ulikuwa mshtuko mkubwa.


Tunashukuru ufadhili wa masomo uliotokana na ushirikiano wa chipkizi wa umoja duniani kote, baadhi ya hao vijana waliweza kwenda shule. Kwa kuona hali yao ya kiafya pale mtaani, tuliandaa 'siku ya Afya': daktari mmoja alitoa muda wake na baadhi ya maduka ya madawa yalitupatia zawadi ya dawa.

Mwezi uliofuata yule daktari alikuja na madaktari wengine watatu. Sasa kule Esmeraldas, mradi unawahusisha hata kina mama wengi wa mahali pale ambao kwa kutaka kutoa muda na mang'amuzi yao, walijenga karakana ya ushonaji.

*(Equador)*



## Kwangu ilitokea...



Tutakuwa na furaha kama...
**tutakuwa na ujasiri wa kugawanya!**

## Kwa undani

# KUMWACHIA MUNGU NAFASI ZAIDI



*Chiara Lubich, Rocca di papa, 20 Juni 1975, Kongamano la gen 3,* Heri

**D**unia inasema heri matajiri na Yesu anasema heri masikini, tena kwa matajiri anasema: «ole wenu, kwa sababu mmeshapata thawabu yenu». Ni kweli, kama kijana mmoja mifuko yake imejaa pesa, kila wakati atafikiri juu ya nini anunue, afanyeje awe na pesa nyingi zaidi ya wenzie na atataka wenzie watamani. Majivuno yanaongezeka na moyo wake hauwi makini kwa sauti ya Mungu na karibu haitawezekana yasimmpate yale ya kijana tajiri wa kwenye Injili ambaye pamoja na kuwa aliitwa na Yesu mwenyewe, hakufaulu kumfuata kwa sababu aling'ang'ania mno mali zake.

Kumbe aliye masikini, haangukii kwenye ulaghai wa kwamba anajitosheleza mwenyewe, bali kwa kujikuta mara nyingi katika uhitaji, huweka tumaini lake kwa Mungu, anajikabidhi kwake na pole pole anagundua kuwa hapati tu like anachoomba, bali anaanza kusiki kuwa Mungu yu karibu naye, tena anakuwa rafiki yake mwenye enzi, ambaye anafanya naye kila kitu na hajisikii kuwa masikini tena bali tajiri na mwenye uhakika.

Wakristo wengi – kwa mfano watakatifu na siku hizi hata wanagen – wameelewa kuwa kummiliki Mungu, si kupokea umasikini kwa upendo, bali ni bora kuwa masikini, yaani, kutong'ang'ania mastarehe ya kuzidi na utajiri unaojaza sana moyo kiasi cha kutoacha nafasi kwa ajili ya Mungu.



Kijana Fransisco wa Assisi, kwa mfano, alikuwa mmoja wa hao. Yeye kwa kuelewa vizuri kwamba utajiri wa baba yake, anasa na ufujaji wa pesa alioufanya na rafiki zake, ulimzuia kumiliki furaha ya kweli, aliwapa masikini kila kitu alichomiliki ili aishi kimasikini na kuwa huru kama ndege. Na Mungu akawa utajiri wake, na kwa furaha kubwa moyo wake ulipaza sauti: «Mungu wangu, kila kitu changu!». Na asingebadilisha kamwe umasikini wake na utajiri wa awali.

**Na hata kwetu gen**, hatupati ile furaha ya kweli tunapoweka vitu vyetu katika ushirika? Kwa hivyo, kati yetu, hakuna anayekosa kile atachohitaji, sote tunacho kile tunachohitaji na ufalme wa mbingu u kati yetu.

*Nota:*
*kwenye wavuti http://assistentigen3.focolare.org pia video inapatikana*

# VYOTE KATIKA USHIRIKA



***Chiara Lubich,***
*Rocca di Papa, 25 Juni 1968,*
Mapinduzi ya Upindemvua

Ningependa kuwaona gen, ninyi gen, wakristo wa karne ya ishirini, wenye uwezo wa kutimiza upeo wa Yesu, kama walivyofanya wakristo wa kwanza.

Hata kama ninyi ni vijana, mtakuwa mlisikia kuwa wakristo wa kwanza waliweka kila kitu shirika. Haikuwa lazima, lakini ushirika wa vitu uliunda sifa yao mojawapo, iliyosikika sana.

Kwa bahati mbaya sisi wakristo wa leo tunakumbuka tu kwamba suala hilo halikuwa la lazima, lakini badala yake hatufikiri kuwa wakristo wa kwanza waliweka kila kitu katika ushirika.

Je, wanagen wanapaswa kufanya nini?

Wasikazie kile ambacho sio cha lazima, bali kile ambacho Mungu anakipenda, anachoweza kukipenda, na kwa kusukumwa na upendo kwake, waweke katika ushirika kila kitu wanachomiliki.

Lakini, kama kuna gen ambaye hajisikii kufanya hivyo asihukumiwe; anaweza hata kutofanya hivyo.

Lakini hii isiwe sheria ya wanagen, bali kitu cha pekee. Sharia inabaki: kuweka kila kitu katika ushirika. Mnaelewa kuwa kama hili litafanyika kati ya maelfu ya gen duniani kote, kutakuwa na mapinduzi.

Ni nani atakuwa aliwahi kuona jambo kama hilo? Vijana wote wajiwekea pesa zao ili kununua michezo, vitabu, kwa ajili ya kujifurahisha.

Ni nani anayefikiri kutumia pesa zake kama mtaji kwa ajili ya wanaohitaji kama walivyofanya wakristo wa kwanza?

Tunataka turudi kwenye mtindo huu wa maisha: ule wa wakristo wa kwanza wa Yesrusalem.

Kizazi kilichopita, narudia, naona kama hakina nguvu: leo ni wachache tu, waliojitoa kabisa kwa Mungu, wanatembea katika mwongozo huu. Lakini kizazi chenu kinaitwa kutokana na mahitaji ya sasa, kuwa wakamilifu katika upeo wa kweli zaidi.

Tutakuwa na furaha kama... tutakuwa na ujasiri wa kugawanya!

## Tutajaribu!

1. Tufanye kwa kuendelea ushirika wa vitu pamoja na gen 3 wengine, kama namna ya kuishi kati yetu utamaduni wa kutoa. Halafu tuamue pamoja ni nini kinahitajika na nini hakihitajiki ili kile cha ziada tumpe anayehitaji zaidi, pia tukiwafikiria gen 3 wengine duniani. Ushirika wa vitu unaweza kutazama tena pesa, vitu vyetu na hata vipaji vyetu na ... muda wetu au hata mahitaji.
2. Pia tunaweza kuandika baadhi ya tafakari au mang'amuzi juu ya utamaduni wa kutoa. Someni pamoja matini zilizoandikwa na chagueni zile zenye mvuto za kuzikusanya katika makala moja na tumeni kwenye ofisi ya uchapishaji ya Teens - email: ***teens@cittanuova.it*** (gazeti lililoandikwa na vijana kwa ajili ya vijana) au kwenye senta kuu ya gen 3: ***gen3m@focolare.org*** na ***centrogen3f@focolare.org*** .
3. Chapisheni karatasi linalohusu utamaduni wa kutoa la kwendanalo baada ya mkutano: itatusaidia tusipoteze mtindo wetu wa maisha ambao msingi wake upo katika ushirika.

## Tupo katika hatua gani?

*Ili **kulifikia lengo** ni lazima kufanya mazoezi kila siku na kutambua mabadiliko mazuri na magumu yaliyojitokeza. Itatusaidia hadi katika mkutano ujao, tutakapotenga muda wa kushirikishana mang'amuzi.*

Tumechagua tarehe ya kuthmini mar kwa mara kama kikundi kile tunachoweza kuweka katika ushirika?

Magumu tuliyokutana nayo

Tulifaulu kueneza kwa vijana wengine nakwenye jumuiya mang'amuzi ya ushirika wa vitu?

Matokeo tuliyoyapata

Kwa ajili ya mlezi

## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kutekeleza umasikini wa roho?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Ni kitu gani cha muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?